**JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MKOA WA DODOMA**

**MTIHANI WA UTAMILIFU KIDATO CHA NNE - 2023.**

**021 KISWAHILI**

**MUDA: SAA 3. Agosti, 2023**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, na C yenye JUMLA ya maswali kumi na moja **(11**).
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A, B, na sehemu C jibu maswali mawili tu **(2).** Swali namba tisa **(9)** ni lazima.
3. Zingatia maagizo ya Kila swali na Kila sehemu.
4. Simu za mkononi haziruhusiwi
5. Andika namba Yako ya Mtihani katika Kila ukurasa wa karatasi ya kujibia

SEHEMU A (Alama 16)

**Jibu maswali yote.**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika kipengele cha (i) - (x) katika maswali yafuatayo:-

i. Musa ni mwanafunzi wa Kidato cha Nne, alialikwa kwenye sherehe ya matambiko na alipata nafasi ya kuongea ili kuelimisha jamii kuhusiana na athari za matambiko na alitoa athari moja ambayo ni

A. Kukuza na kudumaza ubunifu

B. Sherehe husababisha ugomvi na uhasama

C. Hujenga dhana potofu katika jamii

D. Husaidia kukuza uongo na uoga

E. Huongeza hasira kwa mizimu

ii. Kiswahili kilianza kutumika kama lugha ya mawasiliano na kufanywa kuwa lugha ya Taifa nchini Tanganyika wakati gani?

A. Enzi za utawala wa Waingereza

B. Enzi za utawala wa waarabu

C. Baada ya kupata uhuru

D. Baada ya kuingia Wamisionari

E. Enzi za utawala wa Wajerumani

iii. Mwalimu wa Kiswahili alisikika akifundisha wanafunzi namna ya kufuatisha maneno ndani ya sentensi ili kuleta maana sahihi. Kwa kuzingatia sarufi ya Kiswahili Mwalimu alikuwa anafundisha tawi lipi kati ya haya

A. Sarufi mofolijia

B. Sarufi miundo

C. Sarufi matamshi

D. Sarufi maana

E. Sarufi maumbo

iv. Tamthiliya na tanzu nyingine za fasihi andishi hutofautishwa na nini?

A. Ufasaha wa maneno machache

B. Uwezo wa kubeba tanzu nyingine

C. Urari wa vina na mizani

D. Matumizi ya vitendo na mazungumzo

E. Ufasaha wa maneno machache

v. Neno "UTAMLIMISHA" lina fonimu ngapi?

A. 5

B. 11

C. 6

D. 7

E. 3

vi. Ukwapi ni nini katika mshororo wa ushairi

A. Kipande cha pili katika mshororo

B. Vipande vinavyounganisha beti za ushairi

C. Umoja na wingi wa shairi la kimapokeo

D. Ni shairi Tarbia

E. Kipande cha kwanza cha mshororo wa shairi

vii. Mzee Bukuku ana watoto watano, wanne wamebatizwa majina kutoka kwenye nomino za pekee na mmoja amebatizwa jina kutoka kwenye nomino dhahania. Je unafikiri mtoto wa mzee Bukuku ambaye ana jina la nomino dhahania atakuwa nani kati ya hawa;

A. Januari

B. Faraja

C. John

D. Amosi

E. Masanja

viii. Ipi kati ya asasi zifuatazo za kiserikali iliundwa kwa lengo la kukuza na kueneza Kiswahili Zanzibar?

A. BASATA
B. BAMITA
C. BAKIZA
D. BAKITA
E. CHAKIZA

ix. Chukulia umeokota kiboksi kilichojaa vikaratasi vilivyoandikwa vipengele vya maudhui na kuna kikaratasi kimoja tu, kimeandikwa kipengele cha fani, kwa unavyofahamu fani na maudhui unadhani kikaratasi kilichoandikwa kipengele cha fani kitakuwa kina neno gani miongoni mwa maneno yafuatayo;

A. Ujumbe
B. Falsafa
C. Dhamira
D. Msimamo
E. Mandhari

x. Mwanafunzi alifaulu kuendelea na masomo ya ngazi ya Sekondari anatakiwa awe amekamilisha mahitaji muhimu kama vile; sare, daftari na kalamu. Vyote hivi hupatikana ndani ya duka la shule ilihali yeye awe mzima. Neno **ilihali** limetumika kama

A. Nomino
B. Kivumishi
C. Kielezi
D. Kiunganishi
E. Kihisishi

2. Oanisha maneno ya Orodha "A" na Orodha "B" ili kukamilisha maana ya tungo iliyokusudiwa.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| i. TATAKI | A. 1978 |
| ii. BAKIZA | B. 2012 |
| iii. TAKILUKI | C. 1979 |
| iv. BAKITA | D. 2009 |
| v. TUKI | E. 1967 |
| vi. UWAVITA | F. 1970 |

**SEHEMU B (Alama 54)**

**Jibu maswali yote.**

3. Irabu inaweza kubeba hadhi ya silabi katika lugha ya kiswahili. Thibitisha kwa mifano tisa huku ukipigia mstari jibu lako kwa kila mfao.

4. (a) Eleza maana ya lugha.

   (b) Utumiaji wa lugha ni mithili ya Bendera. Jadili kauli hii kwa kutoa hoja tano.

5. (a) Eleza maana ya sarufi.

   (b) Kwa kutumia hoja nne, taja mambo yanayojenga sheria katika lugha ya Kiswahili.

6. (a) Unaelewa nini kuhusu kirai?

   (b) Kwa kupigia mstari, bainisha kirai kivumishi na kirai kielezi

   i. Gari lililoibiwa Arusha limeonekana

   ii. Mwalimu ametufundisha aliyotueleza

   iii. Dada alichukia aliposengenywa

   iv. Mwizi aliyeiba nyumbani amekamatwa

7. (a) Nini maana ya methali.

   (b) Methali hutumia wahusika wanyama kumwakilisha binadamu. Jadili kauli hii kwa kutoa hoja nne (4) mathubuti.

8. Ukiwa kama mtaalamu wa lugha ya Kiswahili nchini, umepokea mwaliko wa kuhudhuria tamasha la Kiswahili dunia linalotarajiwa kufanyika nchii Marekani katika jimbo la New York. Tamasha hilo lipo chini ya usimamizi wa CHAUKIDU, fafanua mchango wa Waarabu walivyosaidia katika kukuza lugha ya Kiswahili.Toa hoja sita ili kuthibitisha madai yako.

**SEHEMU C (Alama 30)**

**Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.Swali namba tisa (9) ni lazima.**

9. Taashira ni nyenzo muhimu anayotumia mwandishi kuifumbua macho jamii. Tumia Diwani mbili kati ya zilizoorodheshwa kuonesha namna waandishi walivyotumia taashira kuzungumza na jamii. ( hoja tatu kwa kila diwani)

10. Mwanamke ni mtu muhimu katika jamii ya watanzania anapokosea jamii hiyo hulegalega.

Jadili nafasi ya mwanamke katika jamii kwa kutumia riwaya mbili kati ya ulizosoma.

11. Waandishi huonesha malalamiko ndani ya jamii zao husika. Thibitisha kauli hii kwa kutumia Tamthiliya mbili ulizosoma. Onesha ni kwanamna gani malalamiko hayo yanaweza kutatuliwa huku ukirejelea vitabu viwili ulivyosoma. Toa hoja tatu kwa kila kitabu.

**ORODHA YA VITABU**

**USHAIRI**

| | |
|---|---|
| Wasakatonge | M.S. Khatibu (DUP) |
| Malenga wapya | TAKILUKI (DUP) |
| Mashairi ya chekacheka | T.A Mvungi (EP&D LTD) |

**RIWAYA**

| | |
|---|---|
| Takadini | Ben J. Hanson (MBS) |
| Watoto wa mama Ntilie | Emmanuel Mbogo (HP) |
| Joka la Mdimu | Abdalah J. Safari (HP) |

**TAMTHILIYA**

| | |
|---|---|
| Orodha | Steve Reynold (MA) |
| Kilio chetu | Medical Aid Foundation (TPH) |
| Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe | Edwin Semzaba (ESC) |